# Utekelezaji wa Sheria za Trafiki

## *Kubadilisha Mbinu za Ofisi ya Liwali ili Kuboresha Usalama Barabarani*

**Imeandaliwa kwa Ushirikiano na:**
Congolese Integration Network, Eastside for All, People Power Washington, Transportation Choices Coalition, na Washington for Black Lives, mradi wa Washington Community Alliance

**Novemba 2025**

King County

OLEO

OFFICE OF LAW ENFORCEMENT OVERSIGHT

# Utekelezaji wa Sheria za Trafiki

*Kubadilisha Utendakazi wa Ofisi ya Liwali Ili Kuboresha Usalama Barabarani*

## Yaliyomo


**Muhtasari wa Utendaji ... 3**

**Utangulizi ... 5**

**Hali ya Usalama na Utekelezaji wa Sheria za Trafiki katika Kaunti ya King ... 8**

- Awamu ya Uhamasishaji ... 8
- Utendakazi wa Ofisi ya Liwali ... 9
- Uundaji wa Mapendekezo ya Sera ... 10

**Mapendekezo ... 11**

- Pendekezo 1 ... 12
- Pendekezo 2 ... 15
- Pendekezo 3 ... 17
- Pendekezo 4 ... 20

**Hitimisho ... 22**

**Maelezo ya ziada ... 23**



**Ripoti imeandaliwa na:**
Simrit Hans, Molly Webster, Lea Hunter, na Katy Kirschner



**Kwa ushirikiano na:** Congolese Integration Network, Eastside For All, People Power Washington, Transportation Choices Coalition, na kwa michango ya Washington for Black Lives, mradi wa Washington Community Alliance.


King County

OLEO

OFFICE OF LAW ENFORCEMENT OVERSIGHT

**King County Office of Law Enforcement Oversight (OLEO) hutoa usimamizi huru wa Ofisi ya Liwali (Sheriff's Office).** Tunafanya mapitio ya kitaalamu yasiyoegemea upande wowote na uchunguzi huru, na kutoa mapendekezo ya sera yanayotegemea ushahidi yakiongozwa na jamii na kuzingatia misingi ya usawa. Ili kutoa mapendekezo haya, OLEO hushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na mashirika ya kijamii.

## Wasiliana na OLEO


Simu: 206-263-8870

Barua pepe: OLEO@kingcounty.gov

Tovuti: kingcounty.gov/OLEO


**Tanbihi kuhusu data:** Kadri inavyowezekana, OLEO imechagua kutumia data maalum za Kaunti ya King ili kuhakikisha usahihi na umuhimu wa matokeo ya utafiti. Hata hivyo, katika hali ambapo data za-ngazi ya kaunti hazipatikani, OLEO inategemea data za-ngazi ya serikali au kitaifa ili kuunda matokeo ya utafiti.


**Ripoti imehaririwa na:**
Liz Dop


**Miundo mbadala inapatikana.**
Piga simu kwa 206-263-8870 au TTY: 711.

# Muhtasari wa Utendaji

## Ripoti Hii: Mbinu na Mchakato Unaongozwa na Jamii

Katika ripoti hii, OLEO na washirika wake wa kijamii wanachunguza utendakazi wa Ofisi ya Liwali katika utekelezaji wa sheria za trafiki na kutoa mapendekezo manne kwa ajili ya kuendeleza mkakati wa utekelezaji wa sheria za trafiki unaotegemea data, unaozingatia usawa, na unaolenga usalama.

Ripoti hii inaashiria Mradi wa kwanza wa Sera Unaongozwa na Jamii ya OLEO—uliokamilishwa kwa ushirikiano na washirika wetu kutoka Congolese Integration Network, Eastside For All, People Power Washington, Transportation Choices Coalition, na kwa michango ya Washington for Black Lives, mradi wa Washington Community Alliance.[a]

Ili kuandaa ripoti hii, OLEO na washirika wake walisikiliza maoni ya watumiaji wa barabara katika Kaunti ya King kuhusu na vipaumbele vyao kuhusiana na hatari za trafiki na mikakati ya utekelezaji wa sheria. OLEO pia ilifanya mahojiano na wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali ili kujifunza zaidi kuhusu sera na mbinu za taasisi hiyo katika utekelezaji wa sheria za trafiki. OLEO ilichambua data za utekelezaji wa sheria za trafiki za Ofisi ya Liwali kwa kipindi cha 2020-2024 ili kuelewa kwa kina hali ya sasa ya utekelezaji wa sheria za trafiki katika Kaunti ya King, na pia ilipitia mbinu bora za kitaifa na mifumo ya sera katika maeneo mengine yanayofanana. Matokeo yote ya utafiti yaliwasilishwa kwa washirika wa OLEO. Mapendekezo manne yanayoongozwa na jamii yaliyotolewa katika ripoti hii yaliandaliwa kwa ushirikiano na kuidhinishwa na washirika wote wa OLEO.

## Hali ya Usalama wa Trafiki na Utekelezaji wa Sheria

Ingawa Ofisi ya Liwali inaona usalama wa trafiki kama kipaumbele, taasisi haina mkakati wa jumla wa utekelezaji wa sheria za trafiki. Badala yake, utekelezaji unaachwa kwa upendeleo wa maafisa binafsi, na kusababisha mbinu isiyo na muundo wa kutekeleza sheria za trafiki. Ofisi ya Liwali haitumi data kwa uthabiti kufahamisha utekelezaji wa sheria za trafiki katika vitengo vyake vyote, na haikusanyi data kamili kwa kila kusimamishwa kwa magari. Hii inamaanisha kwamba Ofisi ya Liwali haina uwezo wa kutathmini kama utekelezaji wake wa trafiki unafanya kazi vizuri au jinsi unavyoweza kuboreshwa. Zaidi ya hayo, kwa kuwa Ofisi ya Liwali haikusanyi taarifa za kidemografia zinazohusiana na kusimaishwa kwa magari, haiwezi kupima iwapo wanatekeleza sheria za trafiki kwa usawa au wanazalisha tofauti au ukosefu wa usawa.

Uchambuzi wa OLEO uligundua kwamba zaidi ya nusu (52%) ya kusimamishwa kwa magari na afisa wa trafiki uliofanywa na Ofisi ya Liwali kati ya 2020-2024 ulikuwa kwa ukiukaji wa trafiki ambapo dereva hakuwakilisha hatari inayoweza kuwadhuru wao wenyewe au wengine, kama vile usajili uliopitwa au taa ya nyuma iliyovunjika. **Matokeo ya OLEO yanaonyesha kuwa kuna fursa kubwa kwa Ofisi ya Liwali kutumia rasilimali chache na kuegemea kwenye mbinu za utekelezaji wa trafiki zinazotegemea data na zinazolenga usalama.**

Watetezi kote Washington, na kitaifa, wanapendekeza kuzingatia rasilimali za utekelezaji wa sheria kwa kupunguza vifo vya barabarani huku wakitambua tofauti za kikabila na kiuchumi zinazotokana na mbinu za kawaida za utekelezaji wa sheria za trafiki. Utafiti unaonyesha kwamba kusimamishwa kwa magari Marekani kunawaathiri zaidi watu wa rangi na jamii zenye kipato cha chini.[1] OLEO na washirika wake walitengeneza mapendekezo katika ripoti hii kushughulikia tofauti katika utekelezaji wa sheria za trafiki na kuboresha usalama wa barabarani kwa watumiaji wote wa barabara katika Kaunti ya King.

---

[a] Soma zaidi kuhusu mchakato wa Mfumo wa Mwongozo wa Jamii hapa..

## Mapendekezo

**1.**

**Kurekebisha miongozo ya sera ili kuipa kipaumbele utekelezaji wa sheria kwa ukiukaji wa trafiki unaohusiana na usalama, kupunguza kusimamishwa kwa magari kwa makosa yasiyo ya usalama, na kuunda mkakati wa utekelezaji wa sheria za trafiki wa taasisi nzima unaoongozwa na data.**

1.1 Zingatia kusimamishwa kunaohusiana na usalama.

1.2 Punguza kusimamishwa kwa magari kusiohusiana na usalama.

1.3 Toa miongozo inayotegemea data kwa maafisa ili kukuza usalama wa barabarani.

1.4 Fuata hatua zisizo za adhabu kushughulikia sababu za msingi za ukiukaji wa trafiki.

**2.**

**Kuweka mipaka kwa maswali na kupiga marufuku upekuzi wa ridhaa wakati wa kusimamishwa kwa magari ili kulinda haki za madereva na kupunguza tofauti za kikabila katika utekelezaji wa sheria.**

2.1 Kuwataka maafisa waweke mipaka ya maswali yao wakati wa kusimamisha gari, kwa kuzingatia sababu kuu iliyosababisha kusimamishwa.

2.2 Kuwataka maafisa kumjulisha dereva mara moja sababu ya awali ya kusimamishwa pindi tu wanapowasiliana naye kwa mara ya kwanza.

2.3 Piga marufuku “upekuzi wa ridhaa” wakati wa kusimamishwa kwa magari.

**3.**

**Kusanya data kwa kila sehemu ya kusimamishwa kwa magari—ikiwemo data za kidemografia—na kutekeleza mbinu bora za ukusanyaji, uhifadhi, na uchambuzi wa data ili kuboresha uwazi na kkuza uwajibikaji.**

3.1 Kusanya na chambua data kwa kila sehemu ya kusimamishwa kwa magari.

3.2 Kusanya na chambua data za kidemografia za kusimamishwa kwa magari.

3.3 Rahisisha mbinu za ukusanyaji wa data.

**4.**

**Iwapo Ofisi ya Liwali inazingatia kuongeza utekelezaji wa trafiki unaotumia mifumo ya kiotomatiki, Kaunti ya King inapaswa kwanza kuagiza utafiti huru wa uwezekano na usawa na kuhitaji ushirikishwaji madhubuti wa jamii kuhusu utekelezaji unaowezekana wa mifumo hiyo.**

4.1 Ofisi ya Liwali haipaswi kuendeleza utekelezaji wa kiotomatiki mpya au wa ziada hadi utafiti wa uhakika na usawa ukapoonyesha njia za kupunguza masuala ya faragha na usawa.

4.2 Mipango yoyote ya baadaye ya utekelezaji wa ziada wa kiotomatiki inapaswa kuongozwa na jamii na kulenga kushughulikia sababu za msingi za changamoto za usalama wa trafiki.

# Utangulizi

## Juhudi za Kutetea Usalama Barabarani Zimekua Katika Miaka ya Hivi Karibuni, Pamoja na Mwelekeo wa Kuongezeka kwa Vifo Barabarani

Ajali za magari ni mojawapo ya sababu kuu za vifo Marekani.[2] Kitaifa, idadi ya vifo barabarani ilipanda wakati wa janga la COVID-19, na ingawa miaka michache iliyopita imeonyesha maboresho polepole katika idadi ya vifo vinavyohusiana na trafiki kitaifa, maendeleo yamekuwa ya polepole katika Jimbo la Washington ambapo vifo barabarani vilifikia kiwango cha juu katika miaka 33 mnamo 2023.[3] Kaunti ya King imeshuhudia mwelekeo kama huo, na ajali 118 zilisababisha vifo katika eneo la mamlaka ya Ofisi ya Liwali kati ya 2020-2024.[b,4]

**33-mwaka kiwango cha juu cha vifo**

Wakati wa janga la COVID-19, maeneo mengi yalipunguza juhudi za utekelezaji wa sheria za trafiki kutokana na kupungua kwa idadi ya magari barabarani na wataalamu wa afya ya umma wakashauri kupunguza mawasiliano kati ya watu kadiri inavyowezekana.[5] Utekelezaji wa sheria za trafiki katika Kaunti ya King ulifuata mtindo sawa, ambapo kiwango cha kusimamishwa kwa magari kulipungua kutoka 2020 hadi 2022 kisha ikaongezeka kwa 40% kati ya 2023 na 2024.[6]

Licha ya kupungua kwa idadi hii, kusimamishwa kwa magari bado ndio muingiliano wa kawaida zaidi kati ya umma na maafisa wa Kaunti ya King,[7] ambapo maafisa walisimamisha magari zaidi ya 87,000 kati ya 2020-2024.[8] Hata hivyo, athari za kusimaishwa huku hakuleti adhari sawa. Kitaifa, utafiti umeonyesha mara nyingi ubaguzi wa rangi na upendeleo wa watu binafsi katika kusimamishwa kwa magari na ukaguzi wa trafiki pamoja na athari zisizo sawa kwa jamii zenye kipato kidogo.[9]

**Trafiki ya Ofisi ya Liwali Iliongezeka mnamo 2024 Ikilinganishwa na Miaka Minne iliyopita**




b "Mamlaka ya Ofisi ya Liwali" inarejelea barabara zinazotunzwa na Kaunti katika maeneo yasiyo ya manispaa ya Kaunti ya King, na barabara zilizoko ndani ya miji yenye mikataba ya Beaux Arts Village, Burien, Carnation, Covington, Kenmore, Maple Valley, Muckleshoot Indian Tribe, Newcastle, Sammamish, SeaTac, Shoreline, Skykomish, na Woodinville. Shirika la Uwanja wa Ndege la Kaunti ya King, Metro, na Sound Transit pia ziko ndani ya mamlaka ya Ofisi ya Liwali.

Kitaifa, na kikanda, watetezi na watunga sera wanajitahidi kutekeleza suluhisho bunifu kufanya barabara zetu kuwa salama zaidi huku wakipunguza utekelezaji wa trafiki usiofaa unaoongeza tofauti za kijamii na kiuchumi.[10] Watetezi wamekuwa wakisisitiza kuwa utekelezaji wa makosa madogo ya trafiki hauboreshi usalama barabarani,[11] kwa kihistoria umetumika kuzingatia jamii za rangi na zenye kipato kidogo na kusababisha matokeo tofauti kwa makundi haya,[12] na pia unazuia afisa kuzingatia makosa makubwa zaidi kama udhaifu wa kuendesha gari, kuendeshwa huku mtu akichanganyikiwa, matumizi ya kamba za usalama, na mwendo kasi, ambazo ndizo sababu kuu za vifo barabarani.[13] Kadri mashirika ya sheria yanavyoongeza uwezo wa kutumia data, kunakuwa na fursa ya kushirikiana na wataalamu wa usalama barabarani kuboresha utekelezaji kulingana na changamoto kuu za usalama barabarani. Teknolojia mpya zinaibuka ambazo—zinapotumika ipasavyo na kwa mwongozo wa jamii—zinaweza kupunguza mzigo kwa rasilimali za sheria na kusababisha kuendesha gari kwa usalama zaidi. Kwa pamoja, utafiti mpya na mbinu bunifu katika maeneo mengine yanaonyesha njia za kuondoa madhara yanayoweza kutokea kutokana na utekelezaji wa jadi wa trafiki na kufanya barabara zetu ziwe salama zaidi.

## Ripoti ya Mkaguzi wa Kaunti ya King Kuhusu Usalama Barabarani

Ofisi ya Mkaguzi wa Kaunti ya King (Ofisi ya Mkaguzi [Auditor's Office]) ilifanya ukaguzi wa mikakati na taratibu za Ofisi ya Liwali kuhusiana na utendakazi wa trafiki mnamo 2022. Ripoti ilibaini kuwa shirika halina mkakati wa jumla wa utekelezaji wa trafiki, na halikadirii kama shughuli za maafisa zinalingana na malengo ya shirika au kuathiri usalama barabarani. Kutokana na matokeo hayo, utekelezaji wa sheria za trafiki unatofautiana katika maeneo yote ya mamlaka ya Ofisi ya Liwali. Ofisi ya Liwali pia haikusanyi kwa mfumo data za trafiki kuhusu kusimamishwa kwa magari wala haichambui iwapo kuna tofauti katika jinsi maafisa wake wanavyosimamia kusimamishwa kwa magari. Kutumia data chache zilizokusanywa, Ofisi ya Mkaguzi iligundua kuwa maafisa Wazungu walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kutumia nguvu dhidi ya madereva Weusi kuliko madereva wa rangi nyingine.

Ofisi ya Mkaguzi iliipa Ofisi ya Liwali mapendekezo matatu kutokana na matokeo yake. Hadi uchapishaji wa ripoti hii, Ofisi ya Liwali haijatekeleza yoyote kati ya mapendekezo haya.

### Pendekezo 1

"Ofisi ya Liwali ya Kaunti ya King inapaswa kubainisha malengo ya utekelezaji wa sheria za trafiki na kuunda pamoja na kutekeleza mikakati ya kufikia malengo hayo, huku ikitumia data kufuatilia maendeleo kuelekea lengo lake kuu la usalama.

### Pendekezo 2

Ofisi ya Liwali ya Kaunti ya King inapaswa kushirikiana na makamanda wa maeneo yasiyo ya manispaa, washirika wa mikataba, na Idara ya Huduma za Mitaa ya Kaunti ya King Kitengo cha Huduma za Barabara (Department of Local Services Road Services Division) ili kuhakikisha kuwa malengo na mikakati ya usalama wa trafiki yanaendana na malengo ya kaunti.

### Pendekezo 3

Ofisi ya Liwali ya Kaunti ya King inapaswa kukusanya data za kidemografia zinazochukuliwa kulingana na mtazamo wa maafisa kwa kila kusimamishwa kwa gari, bila kujali sababu ya kusimamishwa au matokeo yake."

*Soma ripoti kamili hapa.*

## OLEO & Washirika Wake Wafanya Ushirikiano wa Sera Unaoongozwa na Jamii

Kwa kuzingatia kampeni za hivi karibuni za utetezi katika ngazi ya kitaifa na ya jimbo, pamoja na kuongezeka kwa vifo vya barabarani, OLEO na washirika wake walilenga kutathmini na kuboresha mbinu za Ofisi ya Liwali katika utekelezaji wa sheria za trafiki. Ripoti hii inatoa mapendekezo manne ambayo ni matokeo ya Mchakato wa Sera Unaosimamiwa na Jamii ya OLEO,[14] ukiwa umeunganisha mashirika kadhaa ya kijamii kwa jitihada za ushirikiano.

Washirika wa OLEO walichagua utekelezaji wa sheria za trafiki kama lengo la mradi huu kutoka kwenye orodha ya ada tano zinazowezekana za sera. Mradi wa utekelezaji wa sheria za trafiki ulikamilika ndani ya mwaka mmoja na ulijumuisha mashirika matano yanayotegemea jamii: Congolese Integration Network, Eastside For All, People Power Washington, Transportation Choices Coalition, na Washington for Black Lives, mradi wa Washington Community Alliance. OLEO ilikutana na washirika hawa mara kwa mara ili kuwasilisha na kujadili utafiti kuhusu mbinu za sasa za Ofisi ya Liwali, mbinu bora za kitaifa, na mapendekezo yanayoweza kutolewa. OLEO pia ilikutana na wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali na kuchambua data za utekelezaji wa sheria za trafiki zilizopatikana. Baada ya kupitia mapendekezo yanayoweza kutolewa na utafiti unaohusiana, washirika wa OLEO walipiga kura kutoa mapendekezo manne yaliyoorodheshwa katika ripoti hii. Mapendekezo yote manne yalipokelewa kwa kauli moja na mashirika ya kijamii yaliyoishirikiana na OLEO.

## Muda wa mchakato

### 2024

| | |
|---|---|
| SEPTEMBA | Kuanza mikutano na washirika Congolese Integration Network, People Power Washington, Transportation Choices Coalition, na Washington for Black Lives, Washington Community Alliance. |
| OKTOBA | Washirika walichagua utekelezaji wa sheria za trafiki kama mradi wa sera. |
| NOVEMBA | Awamu ya uhamasishaji wa nje-OLEO ilikutana na Ofisi ya Mkaguzi wa Kaunti ya King (King County Auditor's Office) kujadili ukaguzi wao na hali ya mapendekezo yao. Washirika walianza kusambaza Dodoso za Usalama Barabarani na Utekelezaji wa Sheria. |
| DISEMBA | Vikao vya kusikiliza vya ana kwa ana vilifanyika na Congolese Integration Network na Washington for Black Lives. |

### 2025

| | |
|---|---|
| JANUARI | Utafiti ulifungwa baada ya kupokea majibu 187. |
| FEBRUARI-APRILI | Awamu ya utafiti-Mahojiano ya taarifa yalifanyika na wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali katika mamlaka mbalimbali. Data za utekelezaji wa sheria za trafiki zilipokelewa na kuchambuliwa kutoka Ofisi ya Liwali. |
| APRILI | Utafiti na chaguo za sera ziliwasilishwa kwa washirika. Eastside For All ilijiunga kama mshirika wa jamii. |
| MEI | Mikutano na washirika ilifanyika ili kuandaa mapendekezo ya sera. |
| JULAI | Mapendekezo ya mwisho ya sera yaliidhinishwa. |
| AGOSTI-NOVEMBA | Ripoti iliandaliwa na kukamilishwa. Rasimu ya mwisho ya ripoti ilishirikiwa na Ofisi ya Liwali kwa ajili ya mapitio. |

# Hali ya Usalama na Utekelezaji wa Sheria za Trafiki katika Kaunti ya King



## Uhamasishaji: Mtazamo Kuhusu Usalama wa Barabarani na Utekelezaji Wake

Baada ya kubainisha usalama na utekelezaji wa sheria za trafiki kama lengo la mradi, OLEO na washirika wake walianza mawasiliano ili kuelewa jinsi wanajamii wanaoishi, kufanya kazi, na kuendesha magari katika Kaunti ya King wanavyojisikia kuhusu mada hii. Washirika wote wa OLEO walishiriki katika awamu ya uhamasishaji kwa kusambaza dodoso au kuandaa vikao vya kusikiliza maoni ya jamii.

Dodoso, lililotengenezwa kwa ushirikiano na washirika wa OLEO, lilianzishwa Novemba 18, 2024 hadi Januari 7, 2025, na kupokea jumla ya majibu 187. Maswali yote ya dodoso yalikuwa ya hiari, ikiwa na mchanganyiko wa maswali ya kiwango cha Likert na maswali ya majibu ya wazi.[c] Dodoso lilikuwa mtandaoni, na walioshiriki waliweza kulijaza bila kutambulika. OLEO lilishiriki dodoso hilo na washirika wake—ambao waliwasambazia wahusika wao mbalimbali—pamoja na miji yote inayopata huduma chini ya mikataba na Ofisi ya Liwali, na pia kupitia Jarida la Maeneo Yasiyo ya Manispaa la Kaunti ya King (King County's Unincorporated Area Newsletter).

**Washiriki Waliorodhesha Uendeshaji Mbaya wa Magari, Mwendo wa Kasi, na Usalama wa Watumiaji wa Barabara Wasio Tumia Magari Miongoni mwa Wasiwasi Wao Mkuu wa Usalama Barabarani**




Wengi wa washiriki walikuwa wanawake Wazungu wasiokuwa na ulemavu, ambao hawazungumzi lugha nyingine isipokuwa Kiingereza nyumbani—hii haionyeshi jamii mbalimbali za Kaunti ya King, jambo linalopunguza nguvu ya matokeo ya dodoso. Kwa kuzingatia vikwazo hivi, uchambuzi wa OLEO wa matokeo ya dodoso ulitoa baadhi ya taarifa muhimu kuhusu wasiwasi wa watumiaji wa barabara kuhusu usalama wa trafiki. Kwanza, washiriki walitaja uendeshaji mbaya, mwendo kupita kiasi, na usalama wa watumiaji wa barabara wasio na magari kama wasiwasi wao mkubwa zaidi. Pili, takriban theluthi moja ya washiriki waliamini kuwa panapaswa kuwepo na vikwazo vya ziada

---

[c] Kipimo cha Likert ni mfumo wa upimaji unaotumika kupima hisia, mitazamo, na dhana za washiriki kwa kuwauliza washiriki kuchagua kutoka kwa safu ya majibu—kwa mfano, kutoka sikubaliani kabisa hadi nakubaliana kabisa.

kwa ukaguzi wa magari wakati wa kusimamishwa, huku asilimia 12% ya washiriki wakisisitiza kwamba kusimamishwa kunapaswa kufanyika tu kwa sababu halali za usalama, na asilimia 15% wakionyesha kwamba polisi hawapaswi kuuliza maswali zaidi ya sababu ya awali ya kusimamishwa au kufanya kusimamishwa kwa sababu zisizo za kimsingi.[d]

Ili kuendeleza juhudi za ushirikishaji za OLEO kwa mradi huu, mashirika mawili—Congolese Integration Network na Washington for Black Lives, Washington Community Alliance—yaliandaa vikao vya kusikiliza ili kujadili maswali ya dodoso katika mazingira ya majadiliano ya kikundi. Hili liliwawezesha watu waliokosa ufikiaji wa kiteknolojia wa dodoso au waliokuwa wakihitaji huduma za tafsiri kutoa maoni yao na kushiriki uzoefu wao. Vikao kadhaa vya kusikiliza vilifanyika mwishoni mwa Novemba na mwanzoni mwa Desemba mwaka 2024. Kwa kuzingatia hilo, demografia ya idadi ya watu walioshiriki kwenye vikao vya kusikiliza ulitofautiana na ule wa waliojaza dodoso. Congolese Integration Network inahudumia wakimbizi na wahamiaji, hasa kutoka eneo la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Zaidi ya hayo, Washington for Black Lives iliandaa kikao cha kusikiliza kwa akina baba Weusi wanaolea watoto pekee yao.

**Washiriki wa vikao vya kusikiliza walitaja wasiwasi zilizobainishwa na waliojaza dodoso, wakiorodhesha uendeshaji mbaya wa gari, uendeshaji uliosababisha usumbufu, na mwendo kasi kuwa miongoni mwa changamoto kuu za usalama wa trafiki.** Hata hivyo, baadhi ya taarifa zilizokusanywa kutoka kwenye vikao vya kusikiliza zilikinzana na matokeo ya dodoso. Kwa mfano, huku washiriki wa dodoso wakionyesha nia ya kuongezwa kwa maafisa wa sheria katika maeneo yao, washiriki wa vikao vya kusikiliza walishiriki hisia za hofu dhidi ya maafisa wa sheria na kutaka kupunguza mwingiliano nao.

## Utendakazi wa Sasa wa Ofisi ya Liwali

Ili kupata muktadha zaidi kuhusu sera na utendakazi wa Ofisi ya Liwali, OLEO ilifanya mahojiano kadhaa na wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali, kwa kuzingatia vyeo, majukumu, na maeneo mbalimbali. OLEO pia ilishiriki katika ziara za kuambatana na maafisa waliobobea katika utekelezaji wa sheria za trafiki. Mazungumzo haya yaliweka wazi kuwa, licha ya kutaja usalama wa trafiki kama moja ya vipaumbele vya shirika kwa mwaka 2025,[15] Ofisi ya Liwali haina mkakati wazi wa usalama wa trafiki unaoshirikisha shirika lote. Utekelezaji wa sheria za trafiki mara nyingi hubaki kuwa maamuzi ya kila afisa binafsi na zinatofautiana sana kati ya miji yenye mikataba na maeneo yasiyo chini ya manispaa ya Kaunti ya King.[16]

### Matokeo ya Kusimamishwa kwa Magari Katika Kaunti ya King, 2020–2024




Ukosefu wa mkakati au mwongozo wa jumla kuhusu utekelezaji wa sheria za trafiki unasababisha wasiwasi mkubwa. **Yaani, pale ambapo utekelezaji unaachiwa kwa hiari ya maafisa, shirika haliwezi kuhakikisha kwamba wakazi na wageni wa Kaunti ya King wanapata huduma inayolingana na yenye usawa.** Bila mbinu sahihi za ukusanyaji wa data, shirika haliwezi kufuatilia tabia maalum za usalama barabarani na hatua za utekelezaji zinazotokana nazo kote Kaunti ya King. Wasiwasi huu unaendana na kilichogunduliwa na Ofisi ya Mkaguzi katika ukaguzi wao wa 2022 wa utendakazi wa Ofisi ya Liwali.[17]

Ili kuelewa zaidi utendakazi wa sasa wa Ofisi ya Liwali na kuunda ripoti ya Ofisi ya Mkaguzi ya 2022, OLEO ilichambua data za kusimamishwa kwa magari kutoka 2020 hadi 2024. OLEO iligundua kwamba wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali walichukua takriban hatua 112,219 za utekelezaji wa sheria za trafiki na uegeshaji,[e] wakisababisha kusimamishwa kwa magari 87,167. Katika[18] kipindi icho hicho, kusimamishwa kwa magari mbili kati ya tatu kulimalizika kwa onyo. Takriban katika asilimia 25% ya kusimamishwa kwa magari, maafisa walitoa tiketi. Kusimamishwa kwa magari chache sana—asilimia 2% tu—kulimalizika kwa kukamatwa.

---

[d] Usimamishaji wa awali ni pale afisa wa utekelezaji wa sheria anaposimama mtu kwa kosa dogo akiwa na nia ya kufanya upekuzi au kuchunguza kosa kubwa zaidi. Ukaguzi mwingi unaofanywa wakati wa usimamishaji wa magari hautokani na afisa kuwa na kibali au sababu inayowezekana ya kufanya upekuzi huo, bali ni kibali cha dereva.

[e] Hii ni makadirio yanayotokana na uchambuzi wa OLEO wa idadi ya kumbukumbu za utekelezaji zinazohusiana na trafiki katika mfumo wa CAD (Computer Aided Dispatch, Usaidizi wa Usambazaji wa Kompyuta) wa Ofisi ya Liwali. Kumbukumbu moja ya CAD wakati mwingine inaweza kujumuisha vitendo vingi vya utekelezaji, jambo linaloweza kufanya makadirio haya kuwa chini ya idadi halisi.

OLEO ilichambua mara ngapi kusimamishwa kwa magari kunatokea kwa ukiukaji unaohusiana na usalama, ambapo dereva alikuwa akihatarisha maisha yake au ya wengine waziwazi, ikilinganishwa na kusimamishwa kwa makosa ya trafiki yasiyo ya usalama. Ikizingatiwa utekelezaji wote wa sheria za trafiki na za uegeshaji, kusimamishwa kwa magari kwa makosa yasiyo ya usalama kulichangia 52% ya jumla ya hatua zote za utekelezaji zilizofanywa na maafisa wa doria wa Ofisi ya Liwali.

Maeneo yasiyo ya manispaa ya Kaunti ya King, pamoja na Burien, SeaTac, na Sammamish, yalipata idadi kubwa zaidi ya utekelezaji wa sheria za trafiki katika eneo lote la mamlaka ya Ofisi ya Liwali. SeaTac, asilimia 34% tu ya kusimamishwa kwa magari ilikuwa kwa makosa yanayohusiana na usalama, huku Sammamish, asilimia hiyo ikikaribia 60%.

**Ulinganisho wa Ukiukaji wa Sheria za Trafiki Zinazohusiana na Usalama na Zisizohusiana na Usalama Katika Kaunti ya King, 2020-2024**




Kati ya mwaka 2020 na 2024, wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali walitumia nguvu katika kusimamishwa 41 kwa magari, chini ya 0.01% ya jumla ya kusimamishwa kwa magari. Ingawa sampuli ni ndogo, kuna mifumo muhimu inayojitokeza katika data. Katika kipindi icho hicho, 3 kati ya raia 4 waliohusika katika matukio ya matumizi ya nguvu walikuwa wa kiume. Aidha, licha ya kuwakilisha asilimia 7% ya idadi ya watu wa Kaunti ya King,[19] Madereva Weusi walihusika katika asilimia 30% ya kusimamishwa kwa magari kulikohusisha utumizi wa nguvu, jambo linalozua wasiwasi kwamba nguvu inatumiwa kwa kiwango kisicho sawia dhidi ya madereva Weusi.[20]

## Uundaji wa Mapendekezo ya Sera

Kwa kuzingatia msingi na uelewa wa changamoto za sasa katika barabara za Kaunti ya King, OLEO ilichunguza tafiti za kitaifa na mbinu bora za kushughulikia masuala ya usalama wa trafiki, wasiwasi unaohusiana na tofauti za kikabila na kiuchumi katika utekelezaji wa sheria za trafiki, na tathmini za mipango ya usalama na utekelezaji wa trafiki katika maeneo sawia. Sehemu inayofuata ya ripoti hii inawasilisha matokeo makuu ya utafiti huo. Chaguo zinazowezekana za sera za kushughulikia masuala haya ziligawanyika katika makundi manne makuu; kubadilisha sera zinazohusu maamuzi ya utekelezaji wa sheria za trafiki; utekelezaji wa mifumo ya ufuatiliaji wa kiotomatiki; kuhamisha baadhi ya majukumu ya utekelezaji wa sheria za trafiki kwa raia,[f] na kuboresha mbinu za ukusanyaji wa data na ukaguzi ili kuongoza mikakati ya utekelezaji wa sheria za trafiki. OLEO iliwasilisha matokeo haya kwa washirika wake ambao walibainisha mapendekezo ya sera yaliyoainishwa hapa chini ili kuwasilishwa kwa Ofisi ya Liwali

---

[f] Uraia wa kazi unarejelea matumizi ya wafanyakazi raia wasio na silaha kushughulikia ukiukaji wa trafiki badala ya kutumia maafisa wa polisi wenye silaha. OLEO na washirika wake walizingatia utafiti na utetezi wa uraia wa kazi lakini mwishowe waliamua kutotoa pendekezo lolote kuhusu uraia wa kazi katika ripoti hii.

# Mapendekezo

**Mapendekezo manne yafuatayo yaliandaliwa kwa ushirikiano na washirika wa OLEO kwa lengo la kuboresha usalama wa trafiki katika Kaunti yote ya King.**

1. Kurekebisha miongozo ya sera ili kuipa kipaumbele utekelezaji wa sheria kwa ukiukaji wa trafiki unaohusiana na usalama, kupunguza kusimamishwa kwa magari kwa makosa yasiyo ya usalama, na kuunda mkakati wa utekelezaji wa sheria za trafiki wa taasisi nzima unaoongozwa na data.

2. Kuweka mipaka kwa maswali na kupiga marufuku upekuzi wa ridhaa wakati wa kusimamishwa kwa magari ili kulinda haki za madereva na kupunguza tofauti za kikabila katika utekelezaji wa sheria.

3. Kusanya data kwa kila sehemu ya kusimamishwa kwa magari—ikiwemo data za kidemografia—na kutekeleza mbinu bora za ukusanyaji, uhifadhi, na uchambuzi wa data ili kuboresha uwazi na kkuza uwajibikaji.

4. Iwapo Ofisi ya Liwali inazingatia kuongeza utekelezaji wa sheria za trafiki kwa njia ya mifumo ya kiotomatiki, Kaunti ya King inapaswa kwanza kuagiza kufanywa kwa utafiti huru wa uwezekano na usawa na kuhitaji ushirikishwaji mpana wa jamii kuhusu utekelezaji unaowezekana wa mifumo hiyo ya kiotomatiki.

# Pendekezo 1

**Kurekebisha miongozo ya sera ili kuipa kipaumbele utekelezaji wa sheria kwa ukiukaji wa trafiki unaohusiana na usalama, kupunguza kusimamishwa kwa magari kwa makosa yasiyo ya usalama, na kuunda mkakati wa utekelezaji wa sheria za trafiki wa taasisi nzima unaoongozwa na data.**



Watetezi wa Washington, na kitaifa, wanapendekeza kutilia mkazo kusimamishwa kwa magari kunakohusiana na usalama na kupunguza kusimamishwa kwa makosa yanayoweka hatari ndogo kwa usalama wa watumiaji wa barabara.[21] Uangalizi upya katika utekelezaji wa sheria unaohusiana na sababu kuu za vifo barabarani—ikijumuisha uendeshaji mbaya, usumbufu wakati wa kuendesha gari, matumizi ya vifaa vya kidhani, na mwendo kasi—unahitajika kwa haraka kutokana na kuongezeka kwa ajali za kifo na majeraha yanayohusiana na kuendesha gari katika jimbo zima.[22] Kupunguza kusimamishwa kwa makosa madogo kunaweza kuboresha usalama wa trafiki, kurekebisha imani ya jamii, kupunguza uwezekano wa tofauti katika ukaguzi wa polisi, na kupunguza gharama za kifedha zisizo za lazima kwa jamii.[23]

Kitaifa, madhara yanayoweza kutokea kutokana na kusimamishwa kwa magari hayaathiri sawa—madereva Weusi huweza kusimamishwa zaidi kuliko madereva Wazungu, na madereva Weusi na Wahispania wana uwezekano mkubwa wa kufanyiwa upekuzi, kupewa tiketi, kukamatwa,[24] na hata kuuawa wakati wa kusimamishwa kwa gari.[25] Licha ya kutokuwa na ushahidi wa tofauti katika tabia za uendeshaji gari, madereva Weusi wako katika hatari kubwa zaidi ya kusimamishwa kwa makosa madogo au yasiyo ya usalama.[g,26] Marekebisho ya sera yanayolenga kupunguza kusimamishwa kwa magari kwa makosa yasiyo ya usalama yanakusudia kupunguza tofauti katika utekelezaji wa sheria za trafiki kwa kuwapa maafisa miongozo ya kuhakikisha juhudi za utekelezaji zinazingatia ukiukaji unaohusiana na usalama na kupunguza mbinu kama kusimamishwa kwa sababu zisizo dhahiri. Kwa mfano, mwaka 2022, Baraza la Mji wa Philadelphia (Philadelphia City Council) liliweka marufuku kusimamishwa kwa magari kwa baadhi ya makosa madogo yasiyo ya usalama.[27] Baada ya kutekelezwa, kusimamishwa kwa magari kwa madereva Weusi wa kiume kwa makosa madogo kulipungua kwa asilimia 54%—kuirekebisha mtindo ulioandikwa vizuri wa utekelezaji usio sawia huko Philadelphia.[28] Wakati Mkuu wa Polisi Harold Medlock wa Fayetteville, North Carolina, aliwaamuru maafisa wake kuzingatia juhudi za utekelezaji wa sheria za trafiki katika masuala makubwa zaidi ya usalama barabarani na kuacha kusimamisha makosa madogo yasiyo ya usalama, mji huo ulishuhudia kupungua kwa tofauti za kikabila katika kusimamishwa kwa magari pamoja na kupungua kwa ajali za magari, majeraha yanayohusiana na trafiki, na vifo barabarani—yote bila kuathiri makosa yasiyo ya trafiki.[29]

Maamuzi ya utekelezaji wa sheria za trafiki katika Kaunti ya King kwa kiasi kikubwa huachwa kwa hiari binafsi ya kila afisa, jambo linalosababisha mbinu isiyo ya usawa ya usalama wa trafiki katika eneo la mamlaka ya Ofisi ya Liwali. Kama inavyobainishwa katika ripoti ya Ofisi ya Mkaguzi ya 2022, Ofisi ya Liwali haitoi mwelekeo wa kimkakati kwa utekelezaji wa sheria za trafiki,[30] na bila viashiria na malengo yaliyoelezwa, shirika haliwezi kuhakikisha kuwa malengo yake ya utekelezaji yanaweza kufanikisha matokeo yanayohusiana na usalama. Mapendekezo ya OLEO yanakuza mkakati wa utekelezaji wa trafiki unaoongozwa na data unaoelekeza rasilimali chache za shirika kushughulikia masuala makuu ya usalama wa trafiki na kupunguza hatari zinazoweza kutokea kimwili, kiakili na kiuchumi kutokana na kusimamishwa kwa magari.[31]

---

[g] OLEO haina data kamili za kidemografia kuhusu usimamishaji wa magari katika Kaunti ya King. Kulingana na ripoti ya Ofisi ya Mkaguzi ya mwaka 2022, Ofisi ya Liwali haina data za kidemografia za kuchambua tofauti za kikabila katika utekelezaji wa sheria za trafiki. Kwa sasa, taarifa za kidemografia ambazo Ofisi ya Liwali inakusanya si thabiti na haziwezi kutegemewa. Kwa hivyo, katika ripoti hii maelezo kuhusu tofauti za rangi katika utekelezaji wa sheria za trafiki hutegemea data ya kitaifa. See Auditor's Office, "Traffic Enforcement: Strategies Needed to Achieve Safety Goals," 2022, https://kingcounty.gov/en/independents/governance-and-leadership/government-oversight/auditors-office/reports-papers/reports/2022/kcso-traffic-enforcement.

## 1.1 Zingatia kusimamishwa kunaohusiana na usalama.

Lugha ya sera inapaswa kueleza kwamba maafisa wanaweza kusimamisha au kukamata dereva ili kutekeleza ukiukaji wowote wa trafiki unaohusiana na usalama kama ifuatavyo:[h]

a. Ukiukaji wowote wa kanuni za jinai;
b. Ukiukaji wowote unaotokea wakati wa kuendesha gari (ukiukaji unaofanywa na dereva anapoendesha gari, kama vile kuendesha gari vibaya au kwa mwendo wa kasi);[i]
    i. Maafisa hawapaswi kuchukua hatua za kisheria kwa kuendesha gari ikiwa leseni imekataliwa au kusitishwa kutokana na sababu tu za:
        - Hali ya kifedha;
        - Ukiukaji uliofanywa katika jimbo jingine ambao usingepelekea kusitishwa au kukataliwa kwa leseni kama ungefanywa Washington; au
        - Tiketi au taarifa za makosa ya trafiki zilizosababisha kusitishwa kwa leseni za madereva wa kiwango cha kati[j]
c. Ukiukaji wowote wa matumizi ya mkanda wa usalama au vizuizi vya usalama;
d. Ukiukaji wa sharti la madereva kusogea kando au kusimamisha gari kwa magari yenye taa za dharura, ishara za kusimama, au ving'ora.[k]

Lugha ya sera inapaswa pia kueleza kwamba maafisa wanapaswa kusimamisha madereva kwa makosa ya vifaa tu yanayoweka hatari kubwa kwa usalama wa dereva au wengine barabarani ili kutoa elimu au taarifa kuhusu kupata vocha za ukarabati. Ukiukaji wa vifaa unaofikia kiwango cha kuleta hatari kubwa kwa usalama wa dereva au wengine barabarani "una maana kwamba, kwa kuzingatia jumla ya hali zilizopo, ni kawaida kwa mtazamaji wa kimsingi kuamini kwamba ukiukaji huo wa vifaa unaweza kusababisha ajali au kujeruhi dereva au watu wengine au magari yaliyoko karibu. [Hii inaweza kujumuisha]… kuwa taa za nyuma, taa za mbele, au taa za breki hazifanyi kazi au hazionekani wakati wa usiku au pale hali ya hewa inapopunguza mwonekano; kioo cha mbele kilichovunjika kinachomzuia dereva kuona vizuri; au kipumuzi cha kelele kinachovuta chini.[32]

Pendekezo hili halipaswi kuzuia Ofisi ya Liwali kuchukua hatua ya kukamata gari ambalo limeharibika kwa namna inayoweza kusababisha hatari ya papo hapo ya ajali au kujeruhi dereva na wengine walioko barabarani.

## 1.2 Punguza kusimamishwa kwa magari kusiohusiana na usalama.

Sera ya Ofisi ya Liwali inapaswa kusasishwa ili kupiga marufuku kuanzisha kusimamishwa kwa magari kwa ukiukaji usio wa usalama isipokuwa kwa ukiukaji unaohusiana na gari lisilo na nambari ya usajili, au ikiwa nambari ya usajili hailingani na aina, modeli, mwaka, na rangi iliyosajiliwa ya gari, ili kuhakikisha Ofisi ya Liwali inaweza kusaidia katika kupata magari yaliyoibiwa. Ukiukaji usio wa usalama ni ukiukaji wowote wa nyaraka unaohusiana na bima, leseni au ukaguzi, usajili, na ukiukaji wowote wa vifaa ambavyo havileti hatari kubwa kwa usalama wa dereva au wengine walioko barabarani. Maeneo mbalimbali nchini yameanzisha sera sawia, zinazozuia maafisa kuanzisha kusimamishwa kwa magari kwa ukiukaji mdogo. Huko Philadelphia, San Francisco, na Virginia, maafisa hawawezi kuanzisha kusimamishwa kwa magari kwa ukiukaji ufuatao: usajili wa gari umeisha

---

[h] Muundo na maudhui ya pendekezo hili yametolewa kulingana na Mswada wa Bunge wa 1512 (2025).

[i] Kwa ufafanuzi kamili na orodha ya sheria za gari ambazo ukiukaji unaweza kufikia "ukiukaji wa sheria za barabarani unaotokea gari likiwa linaendeshwa," rejelea WAC (Washington Administrative Code, Kanuni ya Utawala ya Washington) 308-104-160, https://app.leg.wa.gov/wac/default.aspx?cite=308-104-160.

[j] Rejelea RCW (Revised Code of Washington, Kanuni Iliyorekebishwa ya Washington) 46.20.342(1)(c) (ii), (v), or (vii), kutoka kwa maandishi ya Mswada wa Bunge uliopendekezwa 1512(2025), Kifungu. 3. (1) (a) (ii), 1512.pdf.

[k] Rejelea RCW 46.37.190, https://app.leg.wa.gov/rcw/default.aspx?cite=46.37.190.

muda wake (kwa nyakati tofauti za muda wa kurahisisha), taa zisizofanya kazi (isipokuwa taa zote hazifanyi kazi), au vitu vinavyopachikwa kwenye kioo cha nyuma.[33] Maeneo mengine yanachukulia ukiukaji ufuatao kuwa ukiukaji mdogo:

a. Rangi za madirisha na vibandiko,[34]
b. Kuhamisha nambari za usajili,[35]
c. Matumizi ya vifaa vilivyoharibika,[36]
d. Kuendesha gari lililojaa kupita kiasi,[37] na
e. Matatizo madogo ya bamba.[38]

## 1.3 Toa miongozo inayotegemea data kwa maafisa ili kukuza usalama wa barabarani.

Ofisi ya Liwali inapaswa kuanzisha rasmi utaratibu wa kutumia vyanzo vipya vya data kama vile mashirika ya trafiki ya manispaa ili kuongoza mikakati ya utekelezaji na kuhakikisha rasilimali zinaelekezwa kwenye masuala ya usalama wa trafiki yenye athari kubwa zaidi. Katika mahojiano na OLEO, wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali walijadili kuhusu kutumia data zilizopo kuelekeza utekelezaji kwenye mizunguko na barabara zilizo na kiwango kikubwa cha ukiukaji wa usalama, kama vile mwendo kasi kupita kiasi au kupita taa nyekundu, lakini mbinu hii haizingatiwi kwa usawa katika shirika na mara nyingi inategemea juhudi binafsi za afisa. Wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali pia walishiriki jinsi shirika linavyoweza kushirikiana na wahandisi wa trafiki na waandaaji miji kutumia data kushughulikia masuala ya muundo wa barabara yanayochangia hali zisizo salama za trafiki.

Uongozi wa Ofisi ya Liwali unapaswa kuendelea kutumia data kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwemo data za usalama wa trafiki, malalamiko ya jamii, na data za kihistoria za utekelezaji, ili kuongoza mikakati ya utekelezaji na kuratibu jitihada za shirika zima za kupima mbinu za utekelezaji na athari zake kwenye matokeo ya usalama wa trafiki. Kuhakikisha maafisa wanapokea maagizo kamili, yanayoongozwa na data kutasaidia kupunguza uwezekano wa upendeleo kuathiri maamuzi ya utekelezaji na kuboresha imani ya jamii.

## 1.4 Fuata hatua zisizo za adhabu kushughulikia sababu za msingi za ukiukaji wa trafiki.

Ofisi ya Liwali inapaswa kushughulikia ukiukaji usio wa usalama kwa hatua zisizo za adhabu zinazoweza kushughulikia sababu msingi ya ukiukaji, badala ya kuongeza matatizo ambayo dereva anaweza kuwa nayo. Kwa mfano, ikiwa dereva hajarekebisha taa ya nyuma iliyovunjika kutokana na ukosefu wa kifedha, kumkamata dereva na kutoza faini kutaongeza mzigo wa kifedha kwa dereva na kunaweza kuchelewesha uwezo wake wa kushughulikia taa hiyo. Imeandikwa vizuri kwamba faini na ada pekee yake si zana bora za kuzuia tabia hasi,[39] na mara nyingi huathiri kwa kiwango kikubwa watu wanaoishi kwa mapato madogo.[40]

Mnamo mwaka 2024, Polisi wa Burien, idara inayofanya kazi kwa mkataba na Ofisi ya Liwali, walifanya ukaguzi wa viti vya watoto 145 na kununua viti vya watoto 45 vilivyotolewa kwa familia zinazo hitaji kupitia ruzuku inayofadhiliwa na serikali. OLEO inahimiza Ofisi ya Liwali kuendelea kuendeleza programu zinazotumia hatua zisizo za adhabu kuwapa madereva vifaa wanavyohitaji ili kuendesha gari kwa usalama barabarani.

# Pendekezo 2

## Kuweka mipaka kwa maswali na kupiga marufuku upekuzi wa ridhaa wakati wa kusimamishwa kwa magari ili kulinda haki za madereva na kupunguza tofauti za kikabila katika utekelezaji wa sheria.

Kupunguza wigo wa maswali ambayo afisa anaweza kuuliza wakati wa kusimamishwa kwa gari na kupunguza uwezo wa afisa kuomba idhini ya dereva kukagua gari lake kunaweza kuelekeza rasilimali chache za Ofisi ya Liwali zaidi kwenye utekelezaji wa ukiukaji unaohusiana na usalama na kupunguza tofauti za kikabila katika utekelezaji wa sheria za trafiki. Ingawa maswali ya uchunguzi yenye wigo mpana na "upekuzi wa ridhaa" ni halali kisheria, mara nyingi huambatana na mbinu za polisi zenye shinikizo na zinazotokana na upendeleo.[41] Kwa mfano, Idara ya Polisi ya San Francisco (San Francisco Police Department) ilitaja kwa uwazi lengo la kupunguza kusimamishwa kwa magari kwa sababu zisizo za msingi kama sababu ya mabadiliko yao ya sera ya hivi karibuni ya kupunguza maswali ambayo maafisa wanaweza kuuliza wakati wa kusimamishwa kwa gari.[42] Wakati maeneo mengi yanapitia mageuzi ya kutumia upekuzi wa ridhaa, Scotland ilipiga marufuku upekuzi kwa sababu ulitumika kwa viwango vya juu mno na kwa kiwango kisicho sawa uliwalenga vijana-wafanyakazi.[43] Baada ya marufuku ya Scotland dhidi ya upekuzi wa ridhaa, ukaguzi uliofanikiwa—ambapo maafisa walipata mali iliyoporwa au dawa za kulevya—uliongezeka na uhalifu ukaelekea kushuka.[44]

Upekuzi wa ridhaa unazua wasiwasi maalum kutokana na jinsi unavyotumika kwa kawaida. Tofauti na aina nyingine za upekuzi,[l] kizuizi cha upekuzi wa ridhaa hakihitaji afisa wa sheria kufikia kiwango cha ushahidi, na kwa hivyo hakuna kiwango kinachohitajika cha ushahidi au uhakika wa kutokea kwa uhalifu. Kuomba ridhaa ya upekuzi kunabaki chini ya hiari ya afisa binafsi na ridhaa ya mtu anayefanyiwa upekuzi.

Licha ya jina lao, watafiti na watetezi wanasema kwamba "upekuzi wa ridhaa hauwi kweli ridhaa ya hiari."[45] Hata pale ambapo haki ya kukataa upekuzi imeelezewa na kueleweka, wasomi wa sheria wanasema kwamba kukubaliana na mtu mwenye mamlaka kama afisa wa polisi si sawa na kutoa ridhaa kwa hiari, na wengi hufanya hivyo kwa kujilinda, wakijua kwamba hawawezi tu kutembea au kuondoka kutoka kwenye tukio hilo na wangekabiliwa na matokeo mengine.[46] Zaidi ya hayo, watu wanyonge, kama vile watoto na wale wenye ulemavu wa akili, wanaweza "kukubali" au kuachilia haki zao za kisheria kwa sababu wanaathiriwa zaidi na wenye mamlaka na hawana uwezekano mkubwa wa kuelewa matekeo kikamilifu.[47]

Mwisho, data za kitaifa zinaonyesha kwamba upekuzi wa ridhaa unafanywa kwa kiwango kisicho sawa dhidi ya madereva wenye weusi, na sehemu kubwa haizalishi kugunduliwa kwa mali haramu.[48] Licha ya kufanyiwa upekuzi wa magari ya madereva Weusi kwa viwango vya juu, viwango vya kugundua mali haramu kwa madereva Weusi ni sawa au vya chini ikilinganishwa na madereva Wazungu.[49] Uchambuzi wa data za kusimamishwa kwa magari pia umebaini kwamba kiwango cha kigezo cha kufanya upekuzi kwa madereva Weusi na Wahispania ni cha chini kuliko kwa madereva Weupe.[50] Wakati baadhi ya wafanyakazi wa sheria wanasema kwamba upekuzi wa ridhaa ni zana muhimu ya uchunguzi, watafiti wamebaini kwamba upekuzi wa ridhaa una uwezekano mdogo wa kugundua mali haramu ikilinganishwa na upekuzi unaofanywa kwa msingi wa sababu zinazowezekana,[m] na hakuna uhusiano kati ya matumizi ya upekuzi wa ridhaa na viwango vya uhalifu wa dhuluma.[51]

---

l I Wakati upekuzi unafanywa chini ya kibali, sababu inayowezekana, au tuhuma zinazofaa, kuna "kiwango cha uthibitisho," au kiwango cha ushahidi, ambacho afisa wa sheria lazima akidhi ili kufanya upekuzi huo. Hii inaunda kiwango sawa na kuweka mamlaka kwa ajili ya vyombo vya sheria wakati vinapoingilia haki ya Ibara ya Nne ya kuwa huru kutokana na ukaguzi usio wa haki.

m Utafiti huu unaonyesha kwamba ukaguzi wa ridhaa ni dhaifu zaidi kuliko ukaguzi unaohitaji kiwango kikubwa cha ushahidi, lakini OLEO pia inatambua kuwa upekuzi unaotegemea sababu za kutenda bila kibali umepigwa marufuku Washington na Mahakama Kuu ya Jimbo. *Jimbo la Washington v. Tibbles (State of Washington v. Tibbles)* (2010).

Licha ya wasiwasi mwingi na muhimu kuhusu utendaji huu, Ofisi ya Liwali mara nyingi hufanya upekuzi wa ridhaa pale inapokuwa "halali na ya maana," lakini haufuatiliwi kwa njia ya kimsingi au inayofikiwa ambayo ingewezesha uchambuzi au uwazi kwa umma.[52] Vivyo hivyo, bila sera za ziada na mafunzo ya tahadhari kuhusu maswali na tabia wakati wa kusimamishwa kwa magari, maafisa wa Ofisi ya Liwali wanaweza kutumia mbinu za uchunguzi zinazohangaisha kwa gharama ya imani na uhusiano na jamii.

## 2.1 Kuwataka maafisa waweke mipaka ya maswali yao wakati wa kusimamisha gari kwa kuzingatia sababu kuu iliyosababisha kusimamishwa.

Ofisi ya Liwali inapaswa kuhakikisha kuwa kusimamishwa kwa magari kunalenga kushughulikia ukiukaji maalum wa usalama wa trafiki, badala ya kutumika kama zana ya uchunguzi wa jumla. Kupunguza maswali wakati wa kusimamishwa kwa gari ili kushughulikia sababu ya kusimamishwa kunahakikisha kuwa maafisa wanachukua hatua kwa tabia hatarishi, jambo linalokuza usalama wa trafiki na elimu kwa madereva. Hata hivyo, lugha ya sera inapaswa kufafanua wazi kwamba ikiwa afisa ana shaka ya kweli kwamba shughuli ya jinai imefanyika, inaendelea, au inakaribia kufanyika, anaweza kuendelea na uchunguzi wa ziada.[53] Pendekezo hili lina lengo la kupunguza kusimamishwa kwa magari kwa sababu zisizo za msingi, ambazo zimebainiwa kuwalenga madereva Weusi kwa kiwango kisicho sawa kitaifa.[54] Kizuizi cha wigo wa maswali hakipaswi kuzuia afisa kuzungumza na dereva kuhusu ukiukaji wa ziada au wa trafiki wa aina mbalimbali ambao anaweza kuwa ameufanya, na hakipaswi kuzuia afisa kumfundisha dereva kuhusu ukiukaji usio wa usalama au kutoa vocha cha ukarabati.

## 2.2 Kuwataka maafisa kumjulisha dereva mara moja sababu ya awali ya kusimamishwa pindi tu wanapowasiliana naye kwa mara ya kwanza.

Miongozo ya sera inapaswa kuweka matarajio ya mawasiliano wazi mwanzoni mwa kusimamishwa kwa gari ili kukuza uelewa kati ya maafisa na madereva na kuboresha uhusiano kati ya vyombo vya sheria na jamii.[55] Kuanzisha kusimamishwa kwa gari kwa heshima na uwazi kunalingana na wajibu wa Ofisi ya Liwali kwa haki za kiserikali na imebainika kuashiria kuaminika kwa wanajamii.[56] Imeandikwa vizuri kwamba kuendesha shughuli kwa kuzingatia kanuni za haki za kiserikali kunaweza kuboresha utii wa hiari na ushirikiano kutoka kwa madereva na kusaidia kuzuia kusimamishwa kwa gari kuongezeka.[57]

## 2.3 Piga marufuku "upekuzi wa ridhaa" wakati wa kusimamishwa kwa magari.

OLEO inapendekeza kwamba Ofisi ya Liwali isitishe matumizi ya upekuzi wa ridhaa wakati wa kusimamishwa kwa magari. Kitendo hicho huzua wasiwasi kadhaa: kulazimisha, tofauti za kikabila katika upekuzi, na kiwango cha ushahidi kinachohitajika kwa upekuzi. Ingawa ni halali kisheria kufanya upekuzi wa ridhaa, wasomi wanasema kwamba upekuzi hauwezi kuwa wa hiari kikweli. Kutokana na wasiwasi huu mkubwa, na ukosefu wa mkakati wa pamoja na data katika Ofisi ya Liwali kuhusu upekuzi wa ridhaa ili kuelewa vyema athari' za upekuzi, OLEO inapendekeza kwamba Ofisi ya Liwali isitishe utekelezaji wa utaratibu huo.

# Pendekezo 3

